

**Learning by Ear 2009
Children's Rights 6
Children's Health**

Topic: Access to healthcare
Author: Mahamadou Koné (Mali)
Editor: Yann Durand
Translator: Anne Thomas
Kkisuaheli: Eric Ponda

	Women	Men	Age	
IN/OUTRO		X	Unimportant	
Narrator	X		Ca. 25	
Mamadou Niafo		X	Ca. 25	
Ali Niafo		X	Ca. 45	
Alkalifa Touré		X	Ca. 40	

LbE Soundtrack

Intro

Hujambo msikilizaji na karibu kwa makala ya sita katika mfululizo wa vipindi vya Learning By Ear Noa bongo Jenga maisha yako tukiwa bado katika maasala ya haki za watoto na juhudi za kudumisha amani.

Leo tunafunga safari hadi nchini Mali ambako huduma za afya kama ilivyo katika mataifa mengi yanayostawi ni duni sana. Watu wenye uwezo

husafiri hadi bara Ulaya au mataifa mengine ambako kuna huduma bora, vifaa na wafanyi kazi wenye ujuzi wa hali ya juu. Lakini ni vigumu kwa watu maskini ambao mara nyingi hutegemea misaada ya matibabu kutoka kwa mashirika ya kujitolea au yasiyo ya kiserikali.

Mamadou Niafo alibahatika kupata msaada wa matibabu kutoka shirika moja lisilo la kiserikali lenye makao yake nchini Ufaransa "Au fil de la vie" – yaani "Kadri maisha yanavyokwenda"

Report

1. OTON : Mdou Niafo 2 (bambara) 12”

"Niliona aibu hata kutembea nje kwa sababu watu walinitazama kila niendapo. Wakati mwengine nilikorofishana na watu hao waliokuwa wakinitazama vibaya."

Narrator:

Mamadou Niafo, mwenye umri wa miaka 25, aliambukizwa maradhi ya kuoza mapua yaani **Noma** akiwa mototo. Ugonjwa huu ni hatari kwani huambukiza watoto midomo na nyuso zao. Mamadou alianza kuugua akiwa mdogo sana. Na chanzo cha matatizo haya yote ni kwa sababu alitoka familia maskini. Babake , Ali Niafo, anataribisha bomani mwake katika wilaya maarufu sana kitongojini mwa mji mkuu wa Bamako nchini Mali..

2. ATMO (In the Niafo concession, there is a small group of men on one side, while women are cooking on the other side, making lunch): 21”

Narrator:

Ali anatueleza jinsi alivyojaribu kumtibu mwanawe wa kiume ambaye alikuwa hajatimia umri wa mwaka mmoja wakati maradhi hayo yalipozuka.

3. OTON: Ali Niafo (bambara): 30”

"Ulikuwa ugonjwa wa ajabu ambao hatukuufahamu kamwe. Sikujua la kufanya. Hivyo nikaamua kutafuta matibabu katika kituo cha afya cha Koutiala yapata umbali wa kilomita 400 kusini mwa mji wa Bamako. Kituo hiki cha afya kilikuwa umbali wa kilomita 15 tu kutoka nyumbani kwangu. Mamadou alikuwa mdogo sana kwamba nilimbeba kwenye boksi kumpeleka hospitalini. Kwa muda wa wiki mbili ilikuwa ni guu na njia, nenda-rudi lakini nikakwama kwa sababu pesa ziliniishia."

Narrator:

Ingawa hakuwa na pesa tena Ali Niafo hakukata tama katika kumshguhulikia mwanawe Kimatibabu. Na njia pekee na rahisi iliyosalia ilikuwa matibabu ya kienyeji.

4. OTON: Ali Niafo (bambara): 22”

"Tulimsafirisha Mamadou hadi kijiji cha Samanyana, sio mbali sana kutoka mjini Bamako, ili kupata matibabu ya kienyeji. Mama mmoja mganga wa kienyeji alifanikiwa kuzuia kusambaa kwa maradhi hayo

hadi sehemu nyingine za mwili wake. Matibabu haya yalisaidia kutuliza uchungu aliokuwa nao lakini tayari alikuwa amepoteza pua yake.

Narrator:

Matibabu ya kienyeji yalizuia kusambaa kwa ugonjwa huu. Ni vizuri kuwa na huduma za aina hii kwani Wa-Afrika wengi hawawezi kumudu gharama za matibabu ya kisasa, kutokana na gharama za madawa yanayotengenezwa katika mataifa yaliyostawi. Hili ni tatizo kubwa hasa katika sehemu za mashambani ambako wakaazi wengi wa sehemu hizi hutegemea sana huduma za madawa ya miti shamba. Pia huduma hizi hutegemewa sana na zaidi ya asilimia 80 ya watu katika mataifa yaliyoko kusini mwa Jangwa la Sahara. Ingawa yaaminika huduma hizi zina uwezo wa kutibu maradhi ya aina mbalimbali, uwezo huo si mkubwa katika kutibu maradhi sugu kama vile ***Noma,***

4. Atmo city sounds

Narrator:

Miaka michache baadaye, familia ya Niafo ilihamia mjini Bamako. Maisha hayakuwa rahisi hasa kwa Mamadou, ambaye alikuwa amepoteza pua yake. Hivyo ilikuwa vigumu kutangamana na

watoto wengine. Baadhi yao walimtoroka, wengine kukataa kula au kunywa naye. Tegemeo kubwa la familia hii lilikuwa mwenyezi Mungu hadi pale walipofahamishwa kuhusu shirika moja lisilo la kiserikali lililokuwa likiwasaidia watu wanaougua maradhi haya. Huo ulikuwa mwaka wa 2006. Na Mamadoua bado anakumbuka:

5. OTON : Mdou Niafo (bambara): 22''

" Tulifahamishwa kuhusu shirika la "Au fil de la vie" na rafiki yetu mmoja ambaye ni muuguzi katika hospital ya Gaabriel Touré mjini Bamako. Alimwambia Babangu kwamba kuna madaktari wa upasuaji wanaoweza kutibu ugonjwa huu noma. Babangu alinipeleka hadi katika hospitali hiyo ambako tulikutana na Daktari Alkalifa Toure ambaye mara moja aliniwekwa kwenye orodha ya wagonjwa wanaosubiri kufanyiwa upasuaji"

Narrator:

Alkalifa Touré ni daktari anayesimamia tawi la shirika hilo nchini Mali ambalo hufanya kazi na washirika kutoka nchini Uswizi na Ufaransa. Madaktari kutoka Ufaransa hufanya upasuaji ilhali wale kutoka Uswizi hufanya kazi ya uuguzi. Wote pamoja na Alkalifa Touré wanaufahamu vyema ugonjwa huu.

6. OTON: Alkalifa 5 (French): 17''

"Watoto walio chini ya umri wa miaka sita wamo hatarini zaidi ya kuambukizwa ugonjwa huu. Kimsingi watoto huambukizwa ugonjwa huu kutokana na Utapiamlo au kutokana na maradhi mengine ambayo hayakuweza kutibiwa vizuri hapo awali na hapo ugonjwa wa Noma huweza kujipenyeza kwa urahisi."

Narrator:

Madaktari kutoka shirika hili la "Au fil de la vie" hutembelea sehemu nyingi za mashambani nchini Mali. Huandaa warsha za kuwahamasisha watu kuhusu kampeni yao dhidi ya ugonjwa huu. Pia huandaa ripoti na takwimu kuhusu idadi ya watoto wanaougua ugonjwa huu. Wakati wataalam kutoka Ulaya wanapowasili, wagonjwa huletwa katika kituo hiki cha afya mjini Bamako ili kufanyiwa upasuaji. Hapa tena ni Alkalifa Touré:

7. OTON : Alkalifa (French): 25''

"Tunawatibu ikiwa wana vidonda,. Wanaweza kupata nafuu katika kipindi cha wiki tatu. Na tunawapa dawa ya spirulina wale wenye upungufu wa damu mwilini. Tusema ni kwa wote. Tunafanya hivi ili kuhakikisha wana kiwango cha kutosha cha haemoglobin kuweza kustahamili upasuaji. Kwa ujumla huongeza uzto wa mwili kabla ya upasuaji kutokana na dawa hiyoy a spirulina.

Narrator:

Mamadou na kundi lake walifanyiwa upasuaji mwaka wa 2007. Operesheni hiyo ilifanyika katika hospitali ya Gabriel Touré mjini Bamako. Anatueleza kilichotokea:

8. OTON : Mdou Niafo (bambara): 23''

"Kwanza kabisa nilidungwa sindano ya genzi na nikapoteza fahamu. Kisha daktari akaanza kuchukua sehemu ya mifupa na ngozi kutoka mwilini mwangu kunitengenezea pua mpya."

9. ATMO (in the Niafo concession, a hen tries to escape and almost falls into the pot on the fire) **Length: 8"**

Narrator:

Mamadou ni miongoni mwa madarzeni ya watoto ambao wameweza kupata tena tabasamu zao baada ya kufanyiwa upasuaji huo. Na kila mwaka idadi ya watoto wanaotibiwa inaongezeka, anasema Alkalifa Touré:

10. OTON : Alkalifa (French): 28"

"Mwaka 2007, tuliwafanyia upasuaji watu 35 , mwaka 2009 watu 55 na mwaka 2009 watu 83. Idadi ilikuwa kubwa mwaka huu kwa sababu tuna kundi jipya la washirika kutoka mataifa ya magharibi waliotaka kutusaidia. Washirika hawa ni pamoja na wawakilishi wa shirika moja lisilo la kiserika nchini Marekani liitwalo "Global Smile""

Narrator:

Wataalam kutoka mataifa ya magharibi hutekeleza jukumu muhimu sio tu kwa kutoa mafunzo bali pia ufadhili. Kwa kweli ni msaada mkubwa sana na wanaziba pengo anasema Alkalifa Touré:

11. OTON: Alkalifa (French): 18"

"Unajua hakuna wodi ya kufanyia upasuaji wa kurekebisha viungo nchini Mali. Kwa hivyo huwa hatuna vifaa vya kutosha. Washirika wetu hutuletea vifaa vyote tunavyohitaji, kila kitu ambacho hatuna na kutuachia sehemu ya vifaa hivyo na kurudi na vingine

Narrator:

Shirika hili limesaidia nchi ya Mali kutimiza ahadi ilizotoa pamoja na mataifa mengine 192 kote ulimwengu kulinda haki za Watoto. Mali ilisaini azimio la Umoja wa Mataifa kulinda haki za watoto la mwaka 1989. Na kifungu nambari 24 kinasema hivi.....

!!!!!!! Use a different voice perhaps for the quote!!!!!!!!!!!!!!!

"Mataifa ni sharti yaheshimu haki za mtoto kufurahia kiwango cha juu cha afya na miundombinuya matibabu kwa magonjwa na kuboresha afya. Mataifa yatafanya juhudi kuhakikisha kuwa hakuna mtoto anayenyimwa haki ya kupata huduma za afya za aina hiyo."

Narrator:

Huduma bora za afya kwa watoto sio tu afya yake ya kimwili bali pia kisaikolojia. Na suala hili halipaswi kupuuzwa hasa ikizingatiwa athari za kisaikolojia zinazosababishwa na ugonjwa huu wa Noma. Na hii ndio sababu shirika la "Au fil de la vie" hufuatilia maisha ya wagonjwa wao hata baada ya upasuaji kuhakikisha kuwa wanaishi maisha ya kawaida na kutangamana na wengine. Huyu hapa tena Alkalifa Touré:

12. OTON: Alkalifa (French): 17"

"Lengo letu si kuwafanyia upasuaji watoto hawa kisha kuwaachilia mbali. Tunafuatilia jinsi wanavyoendelea na maisha yao kwa miaka

au hata miongo baada ya upasuaji. Baadhi ya tuliowatibu wamepata msaada kutoka kwa mashirika mengine na kupelekwa shule

Narrator:

Mamadou hahitaji kujiunga upya na shule. Kwa sababu amekuwa akiendelea na masomo yake licha ya ugonjwa ambao umemrudisha nyuma. Sasa ni mwanafunzi wa mwaka wa tisa na mwenye matumaini makubwa maishani.

13. OTON: Mdou Niafo (bambara): 22”

"Sijaenda shuleni tangu nitoke Hospitalini kwa sababu shule yenyewe iko mbali na nyumbani, na mara nyingi sina usafiri. Afya yangu bado si nzuri sana na ndipo mwalimu mkuu akaniambia kuwa naweza kusomea nyumbani na kwenda kufanya mtihani wangu wa mwisho wa mwaka ."

Narrator:

Leo hii Mamadou ni mwenye furaha na hangepeta kuona watoto wengine wakitaabika kama yeye kutokana na ugonjwa unaoweza kuepukika. Anafahamu kuhusu anachokisema.

14. OTON: Mdou Niafo (bambara): 34”

"Lazima uelewe kwamba ugonjwa wa Noma husababishwa na utapia Mlo, yaani ukosefu wa vitamini. Kwa hivyo ningewahimiza wazazi wote kuwatunza vyema watoto wao. Ugonjwa huu huanza na madoa meusi mdomoni. Halafu viini hushambulia mdomo na pua. Nangewashauri wazazi kusafisha midomo ya watoto wao mara kwa

mara, kuwabadilishia chakula na kuhakikisha wanakula vyakula bora.

ON: Atmo Niafo 2 (in the concession, one woman with a baby is smashing onions in a small mortar. 3-4 meters away two young men are listening to sports news on a local radio. At the end, the baby cries and a man tells him to calm down until his mother is finished.) **Durée : 55''**

NB! Saturated sound at the beginning!!!!

Narrator:

Baada ya mtihani wake Mamadou angetaka kurudi tena michezoni kwani ameikosa kwa miaka kadhaa alipokuwa akiugua. Alikuwa akicheza kandanda na michezo ya kivita kama vile Taekwondo

Music

Narrator:

Hadithi ya Mamadou ni mfano mzuri wa jinsi huduma bora za afya zinavyoweza kubadili maisha ya mtoto. Lakini ni mataifa machache sana yanayoweza kufanya hivyo barani Afrika. Asilimia 10 ya idadi ya watu duniani huishi barani humu ambako asilimia 50 ya vifo vya watoto walio chini ya umri wa miaka 5 huripotiwa katika bara hili. Watoto waliochini ya miaka 5 wamo hatarini zaidi ya kuambukiwa magonjwa na hasa ugonjwa wa Noma. Bara hili halina wepesi wa kuboresha muundo misingi au kuwapa mafunzo zaidi wafanyi kazi wake. Kulingana na ripoti ya shirika la

Afya Duniani ya mwaka 2009, ni mataifa 5 kati ya 49 yaliyoko kusini mwa jangwa la Sahara ambayo yataweza kufikia malengo ya Milenia ya kupunguza idadi ya vifo miongoni mwa watoto waliochini ya umri wa miaka 5 kwa theluthi mbili kufikia mwaka 2015.

End of reportage

OUTRO

Na hadi hapo ndipo tukamilishia kipindi chetu cha leo cha Noa Bongo jenga maisha yako. Kipindi hiki kimetayarishwa na Mahamadou Koné kutoka nchini Mali. Unaweza kukisikiliza tena kipindi hiki kwenye mtandao anwani yetu ni: www.dw-world.de/lbe Hadi wakati mwingine Kwaheri kwa sasa!